



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA AFYA

BARAZA LA WATAALAMU WA MAABARA

Tovuti: [www.hlpc.go.tz](http://www.hlpc.go.tz)



RATIBA YA MTIHANI WA USAJILI-APRILI 2023

Baraza la Wataalamu wa Maabara linawatangazia wataalam wote wa Maabara waliofanya maombi ya Mitihani wa usajili na kukamilisha malipo kuwa tarehe za kufanyika kwa mitihani hiyo ni kama ifuatavyo;

Na	NGAZI YA ELIMU	TAREHE ZA MTIHANI WA NADHARIA	TAREHE ZA MTIHANI WA VITENDO
1	ASTASHAHADA (Certificate)	12.04.2023	13.04.2023
2	STASHAHADA (Diploma)	18.04.2023	19.04.2023
3	SHAHADA (Degree)	24.04.2023	25.04.2023

1. Wote wanaofanya mitihani wanasisitizwa kufika siku ya kwanza ya kuanza Mtihani saa **02:00 Asubuhi** katika vituo cha mitihani kwa ajili ya ukaguzi. **Wafike na Vyeti halisi vya usajili wa awali (Original PRP), Kitambulisho kinachotambulika, Koti la Maabara na vifaa kwa ajili ya mtihani wa nadharia.**
2. Wataalam wote waliofanya malipo ya maombi ya mitihani watapata namba zao za mitihani kupitia akaunti zao za Mfumo wa HPRS walizotumia kufanya maombi ya Mitihani.
3. Wataalam wote wanasisitizwa kutunza barua pepe na nywila (**Email and Password**) zao walizotumia kuomba Usajili wa awali (Provision Registration) kupitia mfumo wa HPRS au zile walizotumiwa na Ofisi ya Msajili kwa ajili ya Kufanya Maombi ya mitihani kupitia mfumo wa HPRS.
4. Wataalam wa Maabara ambao walichelewa kufanya maombi ya Mitihani wa usajili wanashauriwa kufanya maombi ya mitihani Mwezi Oktoba 2023 kwa kuwa dirisha la maombi ya mtihani la mwezi Aprili limeshafungwa na Maandalizi tayari yameshafanyika.
5. Baraza linawatakia Wataalam wote wanaotegemea kufanya mitihani maandalizi na utekelezaji mwema.

Imetolewa na Ofisi ya Msajili

Baraza la Wataalamu wa Maabara

